



## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

### TAARIFA YA MRADI WA MAENDELEO NA UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM (DMDP)

#### 1.0 UTANGULIZI

Mradi wa maendeleo ya Jiji la Dar es salaam (Dar es salaam Metropolitan Development Project) ni mradi unaotekelawa katika Jili la Dar es salaam ukihusisha Halmashauri ya Jiji na Manispaa za Ilala, Kinondoni, Temeke na Ubungo (Awali ulianza na Manispaa tatu za Ilala, Temeke na Kinondoni).

Lengo la mradi huu ni kuboresha miundo mbinu katika Jiji na kujengea uwezo Halmashauri zilizopo katika Jiji la Dar es salaam katika utoaji wa huduma na kujongeza mapato.

Maeneo ya mradi yaliyoainishwa ni pamoja na ujenzi wa barabara zitakazowezesha kupunguza msongamano katika Jiji (Local Roads), kuboresha miundo mbinu katika makazi yasiyopangwa (Infrastructure Upgrading in Unplanned Settlements), kuboresha mifereji ya mvua ili kukabiliana na changamoto ya mafuriko (Storm water drainage), kuweka mifumo ya kisasa ya ukusanyaji wa mapato ( Revenue collection systems) , kujenga uwezo katika miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP Study) na mradi unganishi kati ya miundo mbinu ya usafirishaji na matumizi ya ardhi (Intergrated Transport and Land use Planning).

#### 2.0 MIRADI ILIYOAINISHWA KATIKA MANISPAA ZA KINONDONI NA UBUNGO

Mradi wa DMDP ulianza Mwaka 2010 wakati huo ikiwa ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kabla ya mabadiliko ya kuanzishwa kwa Manispaa mpya ya Ubungo. Baada ya

kazi ya uainishaji wa miradi mbalimbali kufanyika na kupitia hatua za upembuzi wa kitalaam miradi iliyopitishwa ni kama ifuatavyo:-

**1) Barabara (Local Roads)**

Jumla ya barabara zilizoainishwa katika mradi huu ni kumi na moja (11) ambazo ni:-

NA.	JINA LA BARABARA	UMBALI
1.	Makumbusho sokoni	1.45
2.	MMK	0.9
3.	Nzasa	1.2
4.	Tanesco- Msasani Soko la Samaki	1.67
5	Viwandani	2.1
6.	Makanya	5.10
7.	Simu 2000	0.80
8.	Kilimani	1.80
9.	Tandale Kisiwani	1.30
10.	Maji chumvi-Kilungule	3.00
11.	Kilongawima	1.80

Kati ya barabara hizo barabara tano za mwanzo za Makumbusho- Sokoni, MMK, Nzasa, Tanesco Soko la Samaki, na Viwandani ambazo tayari zimeanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara nyingine ni Makanya (Ipo ndani ya Manispaa ya Kinondoni na Ubungo) Kilimani, Kilungule katika manispaa ya Ubungo, Simu 2000 (Ubungo), Tandale- Kisiwani (Kinondoni) na Kilongawima (Kinondoni).

**2) UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU KATIKA MAENEKO YASIYOPANGWA**

Lengo la mradi huu ni kuboresha miundo mbinu katika maeneo yasiyopangwa ambayo yanakaliwa na wananchi wenyewe kipato duni.